**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA**

# YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TANO

***(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)***

**24 NOVEMBA, 2014**

## MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA
## KIKAO CHA KUMI NA TANO – 24 NOVEMBA, 2014

## I. DUA

Mhe. Spika Anne Makinda alisoma Dua saa 3.00 Asubuhi na kuliongoza Bunge

**MAKATIBU MEZANI**

1. Ndg. Charles Mloka

2. Ndg. Laurence Makiji

3. Ndg. Hellen Mbeba

## II. MASWALI

**1. OFISI YA WAZIRI MKUU**

Swali namba 176 – Mhe. Roman Selasini [kny. Mhe. Freeman Mbowe]

Nyongeza i. Mhe. Joseph Roman Selasini
ii. Mhe. Murtaza Ally Mangungu
iii. Mhe. Maryam Salum Msabaha

Swali namba 177 – Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

Nyongeza .1. Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba
2. Mhe. Susan Anselm Lyimo

Swali namba 178 – Mhe. Vicent Josephat Nyerere

Nyongeza i. Mhe. Vicent Josephat Nyerere
ii. Mhe. Ester Amos Bulaya
iii. Mhe. Grace Sindato Kiwelu

## 2. OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)

Swali namba 179 – Mhe. Dkt Henry Shekifu

Nyongeza i. Mhe. Dkt Henry Shekifu

ii. Mhe. Rajab Mbarouk Mohammed

iii. Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya

Swali namba 180 – Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Nyongeza – i. Mhe. Jaku Hashim Ayoub

ii. Mhe Halima James Mdee

Swali namba 181 – Mhe. Agripina Zaituni Buyogera

Nyongeza i. Mhe. Agripina Zaituni Buyogera

Swali namba 182 – Mhe. Eng. Athuman Mfutakamba[Ismail Aden Rage]

Nyongeza – Mhe. Ismaid Aden Rage

## 3. AFYA NA USTAWI WA JAMII

Swali namba 183 – Mhe. Azza Hillaly Hamad

Nyongeza :-i. Mhe. Azza Hillaly Hamad

## 4. WIZARA YA MAJI

Swali namba 184- Mhe. Ezekiel Magolyo Maije

Nyongeza : i. Mhe. Ezekiel Magolyo Maije

ii. James Daudi Lembeli

iii. Mhe. John John Mnyika

Swali namba 185 - Mhe. Mch. Luckson Ndaga Mwanjale

Nyongeza :- i.Mhe. Mch. Luckson Mwajale

ii. Mhe. Aliko Nikusuma Kibona

iii. Mhe. Haroub Shamis Mohammed

**5. MALIASILI NA UTALII**

Swali namba 186 – Mhe. Stephen Hilaly Ngonyani

Nyongeza: Stephen Ngonyani

Swali namba 187 – Mhe. Zabein Muhaji Mhita

Nyongeza: i. Mhe. Zabein Muhaji Mhita

**6. NFUNGO NNA UVUVI**

Swali namba 188 – Mhe. Igras Malocha

Nyongeza. Mhe Ignas Malocha

7. MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali namba 189 – Mhe. David Ernest Silinde

Nyongeza :- i. Mhe David Ernest Silinde

Swali namba 190. – Mhe. Dkt Pudenciana Wlfred Kikwembe

## III. MATANGAZO

1. Wageni wa mke Hussein Mwinyi kutoka jeshi la ulinzi Tanzania
2. Kamati mbalimbali zilitangaziwa kuwa na Vikao saa 7 mchana
3. Kamati ya maendeleo ya jamii na wabunge wote wanawake kitakuwa na semina mchana saa 7 ukumbi wa Msekwa.

## IV. MIONGOZO

1. MMhe. James Mbatia alitumia Kanuni ya 51 kuomba mwongozo kuhusu suala linalohusu Hakli za Bunge alitoa Hoja kuwa Bunge lisitishe shughuli zake zilizokuwa zinaendelea ili kujadili hali iliyojitokeleza kwa taarifa ya CAG kusambazwa mitaani na watu wanaokadiliwa kuwa wameiiba Ofisi ya Bunge jambo ambalo ni kosa chini ya kifungu cha 31 cha sheria ya Haki, kinga na Madaraka ya Bunge.

   Mhe. Spika alimshukuru Mheshimiwa Mbatia na wenzake kutoa taarifa hizo zilizowezesha Bunge na Polisi Kumkamata mtu mmoja ambaye alikuwa anagawa taarifa hiyo.

   Hivyo alitoa maelekezo kuwa Bunge haliwezi kujadili jambo hilo kwa kuwa Polisi wanaendelea kumhoji mtu hivyo ili kupata Taarifa zaidi, na kwamba Bunge litapata fursa ya kujadili mara baada ya kupata taarifa ya Polisi.

   Vilevile Mhe. Spika alieleza kuwa taarifa ya PAC itajadiliwa Bungeni kuanzia tar 26-28-/11/14.

2. Mhe. Mohammed Habib Mnyaa aliomba kiti kiruhusu mjadala wa Hoja itayotolewa na Mhe. James Mbatia kwa sababu ni mjadala mpana kwa kuwa wabunge wanasambaziwa nyaraka mbalimbali zisizo nzuri hadi majumbani mwao.

   KITI. Jambo hili haliwezi kujadiliwa, wasubiri Taarifa ya Polisi

3. Mhe. Tundu Anthipas Lissu alisema kwa kutumia kanuni ya 51(3) Spika baada ya kuridhiha kuwa Hoja iliyotolewa inahusu Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Hoja hiyo inapaswa kupewa kipaumbele katika mpangilio wa shughuli za siku hiyo.

   KITI: Pamoja na kuheshimu taaluma ya Mhe. Tundu Lissu jambo hilo haliwezi kujadiliwa hivi sasa wakati Polisi wanapoendelea na uchunguzi wa jambo husika.

4. Mhe. Christopher Ole-Sendeha aliomba kwamba Taarifa ya CAG pamoja na viambatisho vyake igawiwe kwa Wabunge leo ili wajisomee kabla ya mjadala utakaonza tarehe 26.

   KITI: Utaratibu unafanywa ili Taarifa hiyo igawiwe kwa Wabunge kabla ya siku ya mjadala.

## V. HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Uzuiaji wa Vitendo haramu dhidi ya Usalama wa Miundombinu ya kudumu iliyojengwa chini ya Bahari katika mwambao wa Bara ya mwaka 1998 [*The Protocal for the Suppression of Unlawful Acts against the safety of fixed platforms located on the continental shelf – SUA, 1988*]

- Wajumbe walihoji juu ya Itifaki hiyo na wote kwa Ujumla waliafiki Azimio hilo lilidhiwe .

## VI. HOJA ZA SERIKALI- MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2014 [*The written laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2014*]

- Majadiliano juu ya Muswada huu yaliendendelea kama ifuatavyo:-

3. Mhe. Mbarouk Salim Ali
4. Mhe. Diana Mkumbo Chilolo
5. Mhe. John John Mnyika
6. Mhe.Murtaza Ally Mangungu
7. Mhe. Jenista Joakim Mhagama – NW-Elimu na Mafunzo ya Ufundi

**VII. KUSITISHA BUNGE**

Baada ya kusikiliza mchango wa Naibu Waziri – Elimu Mhe. Spika aliridhika na Hoja iliyotolewa ya kutaka Muswada huu hasa eneo linalopendekeza marekebisho ya Sheria ya Bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu irudishwe kwenye Kamati ili ijadiliwe zaidi; alielekeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii zikutane muda huo kwa ajili ya kazi hiyo.

- Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika alisitisha Bunge hadi saa 11.00 jioni

**VIII. BUNGE KUREJEA**

Bunge lilirejea saa 11.00 jioni na Mhe. Spika aliliongoza.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2014

Majadiliano yaliendelea kwa wabunge kuchangia muswada huo kama ifuatavyo:-

8. Mhe. Margareth Simwanza Sitta
9. Mhe. John John Mnyika
10. Mhe. Ester Amos Bulaya
11. Mhe. Zarina Shamte Madabida
12. Mhe. Jenista Joakim Mhagama
13. Mhe. Prof. Jumanne Maghembe

## IX. KUHITIMISHA HOJA

Mtoa hoja, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali alihitimisha hoja kwa kutoa majibu katika mambo mbalimbali yaliyozungumziwa na Wabunge.

## X. KAMATI YA BUNGE ZIMA

Bunge lilikaa kama Kamati ya Bunge zima na kupitia vifungu vifuatavyo vilivyoandikwa upya 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 8A, 9, 10, 11, 12, 13, 14, 15, 16, 17, 18, 19, 20, 21, 22, 23, 24, 25 na 26.

Kamati ilipokea na kujadili marekebisho kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Murtaza Mangungu, Mhe. Jitu Vrajlal Soni.

Kamati ilipitisha vifungu vyote pamoja na marekebisho yake.

## XI. BUNGE KUREJEA

Bunge lilirejea na mtoa Hoja Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge zima imepitia Muswada kifungu kwa kifungu na kupitisha pamoja na marekebisho kadhaa.

- Baada ya taarifa hii kutolewa Mhe. Spika alilihoji Bunge juu ya Muswada huo ambapo Wabunge walio wengi waliupitisha.

## XII. HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Ushirikiano katika masuala ya Kiulizi (*The East African Protocol on Cooperation in Defence Affairs*)

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mhe. Hussein Ali Misinyi alitoa maelezo juu ya Azimio hilo.

**MAONI YA KAMATI**

Mhe. Vita Rashid Kawawa ambaye ni Mjumbe katika Kamati ya Ulinzi na Usalama aliwasilisha Bungeni Maoni ya Kamati juu ya Azimio hilo kwa niaba ya Mwenyekiti .

**MAONI YA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI**

Mhe. Masoud Abdalla Salim, aliwakilisha Bungeni Maoini ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Azimio hilo.

## XIII. UCHANGIAJI

Wabunge walichangia Hoja hii (Azimio) kama ifuatayo:-

1. Mhe. Anna Margareth Abdallah
2.Mhe. Brig. Gen. (Mst) Hassan Ngwilizi
3. Mhe. Eng. Mohammed Habib Mnyaa
4. Mhe. John John Mnyika

**TANGAZO:**

Mhe. Rajab Mbarouk Mohammed – aliwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa baada ya kuahirisha Bunge.

## XIV. KUHITIMISHA HOJA

Mhe. Hussein Ali Mwinyi alihitimisha Hoja yake kwa kutoa majibu kwa Hoja Mbalimbali zilizotolewa na Wabunge wakati wakichangia na baadaye kutoa Hoja iliyoungwa mkono.

Baada ya Hoja kuungwa mkono Spika alilihoji Bunge juu ya hoja hilo ambapo wote waliunga mkono Azimia hilo.

## XV. KUAHIRISHA BUNGE

Baada ya kukamilisha Shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa siku hii, Mhe. Spika aliahirisha Bunge hadi kesho siku ya Jumanne saa 3.00 Asubuhi.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T.D. KASHILILAH** |
| **24 NOVEMBA, 2014** | **KATIBU WA BUNGE** |